JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI**

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

**Kumb Na. EB.32/160/01/201** **28 Februari, 2025**

Afisa Mtendaji Mkuu,
Sibuka FM Limited,
S.L. P 12702,
**14121 DAR ES SALAAM.**

## UAMUZI JUU YA AMRI YA UTEKELEZAJI

*(Kwa mujibu wa Amri ya Utekelezaji iliyotolewa kwa Sibuka FM Limited tarehe 10 Januari, 2025)*

1.0 **UTANGULIZI**

1.1 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (inayorejewa kama "**Mamlaka**") mnamo tarehe 27 Mei 2010, ilitoa leseni ya Huduma za Utangazaji kwa njia ya Redio (inayorejewa kama "**Leseni**") pamoja na rasilimali ya Masafa ya Redio kwa kampuni ya Sibuka FM Limited (inayorejewa kama "**Mtoa Huduma**") kwa ajili ya utoaji wa huduma za utangazaji.

1.2 Kampuni ya Sibuka FM Limited wakati inapewa leseni na Mamlaka ilikuwa na wanahisa wawili ambao ni:

(a) George Nangalle akimiliki asilinia 50 ya hisa; na

(b) Link Training Centre akimiliki asilimia 50 ya hisa.

1.3 Leseni iliyotolewa kwa Mtoa Huduma ilimtaka Mtoa Huduma, katika kutoa huduma zinzosimamiwa na Mamlaka, kufuata sheria, kanuni, masharti ya leseni na maelekezo ya Mamlaka yanayotolewa mara kwa mara.

1.4 Kanuni ya 39(1) & (2) ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielekroniki na Posta kuhusu Leseni za Mwaka 2018 inamtaka mtoa huduma, ambaye leseni yake inakaribia kuisha muda wake, na mwenye lengo la kuendelea kutuo huduma, kuwasilisha maombi ya kuhuisha leseni kwa Mamlaka, miezi kumi na mbili (12) kabla ya muda wa leseni kwisha.

1.5 Kifungu cha 13(1) cha Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Sura ya 306) kinazuia mtu au kampuni yoyote kutoa huduma za utangazaji nchini bila ya kuwa na leseni toka Mamlaka.

1.6 Kanuni ya 23(1) ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielekroniki na Posta kuhusu Leseni za Mwaka 2018, inamtaka mleta maombi ya leseni au mtoa huduma kutofanya mabadiliko katika muundo wa umiliki wa hisa bila idhini ya Mamlaka.

1.7 Kanuni Kanuni ya 3 ya Kanuni za Mawasiliano ya Kieletroniki na Posta kuhusu Usimamizi wa Vikoa za Mwaka 2020 kama zilizofanyiwa marekebisho mwaka 2023, kinamtaka mtoa huduma yeyote kuhakikisha kampuni yake inatumia kikoa cha dot. tz katika tovuti yake.

1.8 Kanuni ya 5 (a) ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta kuhusu Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni, za mwaka 2018 inamtaka mtoa huduma za utangazaji kuhakikisha anatangaza maudhui mchanganyiko akizingatia tamaduni na mahitaji ya watanzania.

1.9 Kanuni ya 39(2) na (3) ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni za Mwaka 2018 kinamtaka mtoa huduma kuhakikisha anafuata ratiba ya vipindi aliyoiwasilisha kwa Mamlaka na kinamkataza kufanya mabadiliko yoyote bila kuitaarifu Mamlaka.

1.10 Mamlaka katika kutekeleza majukumu yake ya kiudhibiti, ilifanya uchunguzi na kubaini kuwa Mtoa Huduma: -

(a) ameendelea kutoa huduma za utangazaji bila ya kuwa na leseni halali toka Mamlaka tangu tarehe 26 Mei 2015 pale ambapo leseni yake iliisha muda;

(b) pasipo idhini ya Mamlaka, amebadili muundo wa umiliki wa hisa kwa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) kutoka ule wa awali aliowakilisha wakati alipoomba leseni kwenda kwa wanahisa wanne ambao ni:

(i) Boniface Godwin Mwamposa (hisa1638).

(ii) Seleman Godwin Mwamposa (hisa 200)

(iii) Kabeta Godwin Mwasomola (hisa160); na

(iv) George Francis Nangale (hisa 2)

(c) hatumii kikoa cha dot.tz katika tovuti yake;

(d) ameshindwa kuhakikisha anatangaza maudhui mchanganyiko katika matangazo yake ya siku za Jumapili na kushindwa kuzingatia tamaduni na mahitaji ya watanzania; na

(e) ameshindwa kuhakikisha anafuata ratiba ya vipindi iliyoiwasilisha kwa Mamlaka kwa kufanya mabadiliko kwa kurusha maudhui yanayotofauiana katika mitambo yake ya kurusha maudhui iliyopo Simiyu na Dar es salaam.

## 2.0 AMRI YA UTEKELEZAJI

2.1 Mnamo tarehe 10 Januari 2025, Mamlaka ilitoa Amri ya Utekelezaji kwa Mtoa Huduma ikimtaka kuwasilisha utetezi wake kimaandishi na kufika katika ofisi za TCRA Makao Makuu Dar es Salaam tarehe 22 Januari 2025, saa tano (5:00) asubuhi kujieleza kwa nini asichukuliwe hatua za kisheria kwa:

(a) kuendelea kutoa huduma za utangazaji bila ya kuwa na leseni halali toka Mamlaka kinyume na Kifungu cha 13(1) ya Sheria ya Mawasiliano ya Kielekroniki na Posta (Sura 306);

(b) kubadili umiliki wa hisa pasipo idhini ya Mamlaka kinyume na Kanuni ya 23(1) ya Kanuni za Sheria ya Mawasiliano ya Kielekroniki na Posta kuhusu Leseni za Mwaka 2018;

(c) kutotumia kikoa cha dot.tz katika tovuti yake kinyume na kanuni ya 3 ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroki na Posta kuhusu Usimamizi wa Vikoa za Mwaka 2020 kama zilizofanyiwa marekebisho mwaka 2023;

(d) kushindwa kuhakikisha anatangaza maudhui mchanganyiko katika matangazo yake ya siku za Jumapili na kushindwa kuzingatia tamaduni na mahitaji ya watanzania kinyume na kanuni ya 5 (a) cha Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta kuhusu Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni, za Mwaka 2018; na

(e) kushindwa kuhakikisha anafuata ratiba ya vipindi aliyoiwasilisha kwa Mamlaka kwa kufanya mabadiliko kwa kurusha maudhui yanayotofauiana katika mitambo yake ya kurusha maudhui iliyopo Simiyu na Dar es salaam bila kuitaarifu Mamlaka kinyume na kanuni ya 39(2) na (3) ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta kuhusu Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni za Mwaka 2018.

## 3.0 KUSIKILIZWA KWA UTETEZI

3.1 Mtoa Huduma alifika Ofisi za Mamlaka tarehe tarehe 22 Januari 2025 tarehe iliyokuwa imepangwa kwa usikilizwaji na kuomba ahirisho kwa madai kuwa wito wa Amri ya Utekelezaji ulikuwa haujamfikia. Ndipo Mamlaka ilipanga kumsikiliza Mtoa Huduma tarehe 29 Januari 2025;

3.2 Tarehe 29 Januari Mtoa Huduma alifika kwa usikilizwaji akiwakilishwa na Bwana Andrew Chaopa ambaye ni Maneja wa kituo cha redio akiambatana na Bi. Editha Oby ambapo waliweza kutoa utetezi wao kwenye baadhi ya hoja na kuomba waendelee na utetezi wao tarehe 06 Februari 2025; na

3.3 Tarehe 06 February Mtoa Huduma alifika kuendelea na utetezi wake akiwakilishwa na Bwana Michael Kabeta Mkurugenzi Mtendaji akiwa pamoja na Bwana Andrew Chaopa na Bi. Editha Oby. Pamoja na utetezi wa maandishi, waliwasilisha kama ifuatavyo:

3.4 **Kuhusu kuendelea kutoa huduma za utangazaji bila ya kuwa na leseni halali toka Mamlaka kinyume na Kifungu cha 13(1) ya Sheria ya Mawasiliano ya Kielekroniki na Posta;**

Mtoa Huduma alikiri kuwa leseni yao imeisha muda wake na mara kadhaa wamekumbushwa na Mamlaka kuhuisha leseni hiyo. Aliwasilisha zaidi kuwa, hata hivyo, wameshawasilisha maombi ya kuhuisha leseni katika mfumo wa Tanzanite Portal tangu tarehe 09 Januari 2025.

3.5 **Kuhusu kubadili umiliki wa hisa pasipo idhini ya Mamlaka kinyume na Kanuni ya 23(1) ya Kanuni za Sheria ya Mawasiliano ya Kielekroniki na Posta kuhusu Leseni za Mwaka 2018;**

**3.5.1** Mtoa Huduma aliwasilisha kuwa tarehe 01 Februari 2022 waliwasilisha maombi Mamlaka kuomba idhini ya kubadili mundo wa umiliki wa hisa katika kampuni ya Sibuka FM Limited. Mamlaka iliwajibu na kuwapa namba ya malipo CN 991060033926, ambapo tarehe 07 Januari 2022 waliweza kulipa Dola za Kimarekeani (USD)1500. Na baada ya kufanya malipo hayo ndipo walienda kwa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) kubadili muundo wa umiliki wa hisa.

3.5.2 Aliendelea kuwasilisha kuwa, Octoba 2022 walirejea Mamlaka ili kuleta nyaraka za BRELA zinazoonyesha muundo mpya wa umiliki wa hisa. Hata hivyo, walijulishwa kuwa mabadiliko ya hisa yalipaswa kufanywa katika kampuni ya Sibuka Media Limited na si Sibuka FM Limited.

3.5.3 Mtoa Huduma aliwasilisha kuwa, kwa kuwa alijua kuwa, Sibuka Media Limited alikuwa amepewa uendeshaji wa redio pekee na si umiliki, na kwa kuwa hakuwa na nyaraka za Mamlaka za kuruhusu mabadiliko ya menejiment ya Redio ya Sibuka FM aliondoka na kwenda kutafuta nyaraka husika. Ilichukua muda kidogo, mwaka 2024 alifanikiwa kupata nyaraka za Mamlaka zilizoridhia kuhamisha menjementi ya redio kutoka Sibuka Ltd kwenda Sibuka Media Ltd.

3.6 **Kuhusu kutotumia kikoa cha dot.tz katika tovuti yake kinyume na kanuni ya 3 ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroki na Posta kuhusu Usimamizi wa Vikoa za Mwaka 2020 kama zilizofanyiwa marekebisho mwaka 2023**;

Mtoa huduma aliwasilisha kuwa tayari ameshafanya usajili wa tovuti yake tangu October 2024 inayotumia kikoa cha dot. Tz inayojulikana kwa www.sibukafm@c.tz

3.7 **Kuhusu kushindwa kuhakikisha anatangaza maudhui mchanganyiko katika matangazo yake ya siku za Jumapili na kushindwa kuzingatia tamaduni na mahitaji ya watanzania kinyume na kanuni ya 5 (a) cha Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta kuhusu Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni, za Mwaka 2018;**

3.7.1 Mtoa Huduma aliwasilisha kuwa, katika Mpangilio wa Vipindi (Program Line up), aliyowasilisha Mamlaka ameonyesha vipindi mchanganyiko vinavyorushwa siku ya jumapili kuwa ni:

(i) Shuhuda na Matendo Makuu (Asubuhi saa 11-12)
(ii) Habari (saa 01 Asubuhi)
(iii) Mahubiri (saa 3 Asubuhi – 9 alasiri)
(iv) Mezani Leo (saa 9 alasiri -10 jioni)
(v) Mahubiri (10 Jioni – 2 Usiku)
(vi) DJ Playlist (saa 2 – 2:30 usiku)
(vii) Habari (saa 2:30 – saa 3 usiku)
(viii) Mahubiri (Saa 3-5 usiku)
(ix) Gospe; Zilipendwa (saa 5-8 usiku)

3.8 **Kuhusu kushindwa kuhakikisha anafuata ratiba ya vipindi aliyoiwasilisha kwa Mamlaka kwa kufanya mabadiliko kwa kurusha maudhui yanayotofauiana katika mitambo yake ya kurusha maudhui iliyopo Simiyu na Dar es salaam bila kuitaarifu Mamlaka kinyume na kanuni ya 39(2) na (3) ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta kuhusu Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni za Mwaka 2018.**

Mtoa Huduma alieleza kuwa pale ambapo studio zilizopo Dar es Salaam zinapopata hitilafu za kiufundi kama changamoto ya umeme, ndipo studio ziilizopo Simiyu huwa wanaendelea kwa mfumo wa kujiunga vya moja kwa moja kutoka huko yaani *hook up.* Alieleza kuwa kati ya mwezi Aprili mpaka Juni 2024 walipatwa na changamoto hiyo kwa vipindi vya asubuhu lakini kwasasa wamerekebisha. Na aliomba msamaha kwa changamoto hizo.

**4.0 UZINGATIAJI WA UTETEZI**

Baada ya kupitia utetezi wa Mtoa Huduma uliowasilishwa kwa maandishi na kwa mdomo, Mamlaka imezingatia utetezi huo kama ifuatavyo:

4.1 **Kuhusu kuendelea kutoa huduma za utangazaji bila ya kuwa na leseni halali toka Mamlaka kinyume na Kifungu cha 13(1) ya Sheria ya Mawasiliano ya Kielekroniki na Posta;**

**4.1.1** Mamlaka imezingatia kuwa Mtoa Huduma amekiri kuwa amekuwa akitoa huduma za utangazaji bila kuwa na leseni, pamoja na kukumbushwa mara kadhaa.

**4.1.2** Kuhusu utetezi wa Mtoa Huduma kuwa ameshawasilisha maombi ya kuhuisha leseni hiyo tangu Januari 09, 2025; Mamlaka inatambua kuwa, Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta zinazohusu Leseni za mwaka 2018 zinamtaka Mtoa Huduma ambaye leseni yake inakaribia kufikia mwisho, kuwasilisha maombi ya kuhuisha leseni endapo anahitaji kuendelea na utaoaji wa huduma, miezi kumi na mbili (12) kabla ya muda wa leseni yake kuisha. Mtoa Huduma leseni yake iliisha tangu tarehe 26 Mei 2015, hivyo basi, alipaswa kuwasilisha maombi hayo tarehe 26 Mei, 2014 kitu ambacho alishindwa kufanya na hivyo kuendelea kutoa huduma kwa muda wa takribani miaka tisa (9) bila kuwa na Leseni halali.

4.2 Kuhusu kubadili umiliki wa hisa pasipo idhini ya Mamlaka kinyume na Kanuni ya 23(1) ya Kanuni za Sheria ya Mawasiliano ya Kielekroniki na Posta kuhusu Leseni za Mwaka 2018, Mamlaka imepitia kumbukumbu za taarifa za Mtoa Huduma na kujiridhisha na utetezi wa Mtoa Huduma kuwa alipata idhini ya Mamlaka kabla ya kufanya mabadiliko ya muundo wa umiliki wa hisa kwa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni.

4.3 Kuhusu kutotumia kikoa cha dot.tz katika tovuti yake kinyume na kanuni ya 3 ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroki na Posta kuhusu Usimamizi wa Vikoa za Mwaka 2020 kama zilizofanyiwa marekebisho mwaka 2023, Mamlaka pia imejirisha kuwa Mtoa Huduma ameshafanya usajili wa tovuti yake na sasa anatumia kikoa cha dot.tz.

4.4 Kuhusu kushindwa kuhakikisha anatangaza maudhui mchanganyiko katika matangazo yake ya siku za Jumapili na kushindwa kuzingatia tamaduni na mahitaji ya watanzania kinyume na kanuni ya 5 (a) cha Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta kuhusu Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni, za Mwaka 2018, Mamlaka ilibaini kuwa Mtoa Huduma, pamoja yakuwa aliwasilisha mpangilio wa vipindi ukionesha kuwa na maudhui ya habari, katika ufuatiliaji wa maudhui yanayorushwa siku ya jumapili, ni dakika arobaini (40) tu ndizo hutumika kurusha maudhui ya habari kinyume na matakwa ya Kanuni.

4.5 Kuhusu ukiukaji wa kanuni ya 39(2) na (3) ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta kuhusu Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni za Mwaka 2018, Mamlaka imezingatia kuwa, Mtoa Huduma amekiri kurusha maudhui yanayotofautiana katika mitambo yake ya kurusha maudhui iliyopo Simiyu na Dar es Salaam bila kutoa taarifa kwa Mamlaka. Utetezi wa Mtoa Huduma kuwa alipata changamoto ya umeme; Mamlaka inatambua kuwa Mtoa Huduma anapaswa kuwa na mifumo ya umeme mbadala kama magenereta ili kuhakikisha kuwa anaweza kutoa huduma muda wote.

5. **UAMUZI**

5.1 Baada ya kusikiliza na kuchambua utetezi wa Mtoa Huduma, Mamlaka imejiridhisha kuwa Mtoa Huduma amekiuka:

a) Kanuni ya 39 ya Kanuni za Sheria ya Mawasiliano ya Kielekroniki na Posta kuhusu Leseni za Mwaka 2018; kwa kuendelea kutoa huduma za Utangazaji pasipo kuhuisha leseni;

b) Kanuni ya 5 (a) cha Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta kuhusu Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni, za Mwaka 2018; kwa kushindwa kuhakikisha anatangaza maudhui mchanganyiko katika matangazo yake ya siku za Jumapili; na

c) Kanuni ya 39(2) na (3) ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta kuhusu Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni za Mwaka 2018; kwa kushindwa kuhakikisha anafuata ratiba ya vipindi aliyoiwasilisha kwa Mamlaka kwa kufanya mabadiliko kwa kurusha maudhui yanayotofautiana katika mitambo yake ya kurusha maudhui iliyopo Simiyu na Dar es salaam bila kuitaarifu Mamlaka.

**HIVYO BASI,** kwa mujibu wa kifungu cha 114 cha Sheria ya Mawasiliano na Kieloctroniki na Posta [Sura ya 306], pamoja na Kifungu cha 48 (2) na (3) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania [Sura ya 172], TCRA inatoa **ONYO** kwa **Sibuka FM Limited** kwa ukiukaji sheria, kanuni na masharti ya leseni na **KUIAMURU Sibuka FM Limited** kukamilisha mchakato wa kuhuisha leseni; na

**ENDAPO Sibuka FM Limited** itarudia ukiukaji wa sheria, kanuni na masharti ya leseni kuhusu maudhui ya utangazaji, Mamlaka itaendelea kuchukua hatua zaidi za kisheria na kiudhibiti ikiwemo kusimamisha au kufuta leseni na kunyang'anya masafa.

Amri imetolewa tarehe...............ya mwezi Februari, 2025.

Digitally Signed By JABIRI KUWE BAKARI
Fri Feb 28 22:51:50 EAT 2025

Dkt. Jabiri K. Bakari
**MKURUGENZI MKUU**

Amri hii imepokelewa na **Sibuka FM Limited** tarehe..03......mwezi Machi, 2025 na:

Jina: ANDREW M. CHAOPA

Cheo: MENEJA

Sahihi: ..........................

RADIO SIBUKA FM P.O. BOX DAR-ES-SALAAM

(Muhuri wa Ofisi)